# Sababu za Mkengeuko wa Malezi kwa Wahusika katika Riwaya ya *Rosa Mistika*

*Selestino Helman Msigala*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

**Ikisiri**

**Ingawa wahusika hukengeuka malezi, wataalamu na wachambuzi hutofautiana katika kuelezea jambo hili. Wapo wanaoona kuwa, kukiuka malezi kwa wahusika katika kazi za fasihi kunasababishwa na wazazi au walezi (Wanjala, 2015; Mbatiah, 2016; Doepke na Zilibotti, 2019). Kwa upande mwingine, wapo wataalamu wanaowatupia lawama watoto kuwa wanabadilika hasa wanapotoka mikononi mwa wazazi na kuingia katika jamii kutokana na kushindwa au kupuuza malezi na maelekezo kutoka kwa wazazi au walezi wao (Ondieki, 2015; Jonas, 2017). Aidha, upande mwingine jamii hulaumiwa kwa kushindwa kuendeleza malezi yanayofaa kutoka kwa wazazi au walezi wa watoto (Mitchell, 2010; Martin, 2017; Sanga, 2018). Tofauti hizi za kimtazamo ndizo zilizosukuma kuandikwa kwa makala hii. Kwa hivyo, makala hii inakusudia kujadili sababu za mkengeuko wa malezi kwa wahusika kwa kutumia riwaya ya Rosa Mistika (Kezilahabi, 1971).**

**Maneno Muhimu:** Riwaya, Kukengeuka, Malezi, Nadharia ya Sosholojia

## Utangulizi

Malezi ni jambo muhimu kwa ustawi wa jamii kwani hutarajiwa kutoa maadili yaliyo katika jamii (Mbatiah, 2012; Wanjala, 2015; Beebee 2016). Mathalani, Wanjala (2015) anaeleza jinsi malezi kwa wahusika yanavyoathiri utambulisho wa vijana katika riwaya ya Kiswahili. Mawazo yake yanaonesha kuwa ili vijana wapate maadili ya jamii zao wanapaswa kupata malezi yanayofaa. TUKI (2014) inafafanua kuwa malezi ni njia ya ukuzaji wa mtoto kwa kutarajiwa kufuata tabia na mwenendo unaostahiki. Wapokeaji na watoaji wa maelekezo ya kimalezi wanapokiuka kutoa au kupokea maelekezo ya kimalezi, huweza kusababisha kinachotarajiwa katika malezi hayo kutofikiwa. Hali hii katika makala hii ndiyo inatazamwa kama mkengeuko wa malezi.

Wanajamii huhitajika kuwa na malezi yanayokubalika ili kuondoa migogoro na changamoto mbalimbali (Mahonge 2016). Mlacha (1986) anafafanua kuwa wahusika wanaotumika katika kazi za nathari za Kiswahili mara nyingi huwa ni vijana ambao ni wapya katika jamii zao na kwa upande mwingine huwa katika umri wa kuanza kujitegemea. Vijana hawa hujitenga na jamii zao kutokana na kuwa katika umri wa kutaka uhuru katika maamuzi. Aidha, wapo vijana wengine ambao wamepata utamaduni wa elimu ya Kimagharibi ambao ni tofauti na utamaduni wao asilia. Utamaduni huo wa kigeni unaonekana kuwa tofauti na utamaduni asilia wa jamii na hivyo kusababisha mgogoro wa malezi katika jamii kwa sababu huwa wamekengeuka.

Fauka ya hayo, wapo wataalamu wanaoona kuwa mazingira ya kijamii huweza kumsukuma mhusika kuyakengeuka malezi (Durisic na Bunijevac, 2017). Mathalani, Wamitila (2008) na Madumulla (2009) wanadokeza mkengeuko wa wahusika katika aina za riwaya za Kiswahili wanazozijadili. Wamitila (2008) anapoelezea aina za riwaya, anagusia riwaya ya ukuaji inayojifunga kwenye maisha ya mhusika ambaye anachunguzwa tokea utotoni au ujanani hadi utu uzima.

Mkengeuko wa malezi unaweza kusawiriwa katika kazi za fasihi ikiwamo riwaya (Mbatiah 2012). Hata hivyo, ingawa malezi hutolewa kupitia kazi mbalimbali za fasihi, bado baadhi ya wahusika wanaotumiwa katika kazi za fasihi ikiwamo riwaya, huchorwa kuyakengeuka malezi hayo (Wamitila, 2008 na Madumula, 2009). Ukiukaji wa malezi unaweza kusawiriwa katika kazi za fasihi kwa sababu fasihi ni zao la jamii (Mulokozi, 2017). Kwa hiyo, makala haya yanakusudia kuchunguza sababu za mkengeuko wa malezi katika riwaya ya *Rosa Mistika*.

## Vyanzo vya Data na Msingi wa Kinadharia

Data za makala hii zimekusanywa kwa njia ya mapitio ya nyaraka za maktabani pamoja na udurusu wa matini ya riwaya ya *Rosa Mistika*. Uchambuzi wa data umeongozwa na Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi. Nadharia hii imeteuliwa kwa sababu inashikamanisha jamii na kazi za fasihi. Nadharia hii inaelezwa na Coser (1963) kuwa iliasisiwa na Charles Taylor (1822-1917) na Georg Lukacs (1885-1971). Kutokana na nadharia hii, fasihi na sanaa ni picha ya uhalisi katika jamii. Kwa namna nyingine, Hallen (1966) akieleza kuhusu fasihi na jamii anadai kuwa fasihi ni taswira, mwongozo na kishawishi cha mabadiliko katika jamii. Tukiisoma na kuichambua kazi ya fasihi tunaweza kupata picha halisi ya jamii husika (Carter na Carter, 2014; Titus, 2018,).

Nadharia hii imetusaidia kukusanya na kuchambua data za riwaya ya *Rosa Mistika* (Kezilahabi; 1971). Riwaya hii imeteuliwa kwa kuzingatia uchunguzi wetu wa awali uliobaini kuwa ni riwaya ya kiuhalisia, katika mkondo wa riwaya za ukuaji ambazo zinamuonesha mhusika tangu anakuwa mdogo hadi mtu mzima. Riwaya hii pia imeonesha kuwa na kiwango kikubwa cha wahusika wanaokengeuka malezi.

## Sababu za Mkengeuko wa Malezi kwa Wahusika katika Riwaya ya *Rosa Mistika*

*Rosa Mistika* ni riwaya ya kihalisia iliyoandikwa na Euphrase Kezilahabi mwaka 1971. Simulizi ya riwaya hii imejengwa kwa mhusika Rosa Mistika na familia yake. Rosa analelewa kwa ukali, tangu akiwa mdogo. Hata hivyo, Rosa anabadilika na kuwa malaya baada ya kufika sekondari na chuoni. Baada ya kumaliza ualimu, anapangiwa kufundisha Mkoa wa Mwanza ambako anaanza mahusiano ya mapenzi na Charles na kukubaliana kuoana. Hata hivyo, uchumba wao unavunjika baada ya Rosa kukutwa si bikra; na anapogundua kuwa ameachwa na Charles, anaamua kujiua.

Kwa jumla, riwaya imethibitisha kuwapo kwa sababu mbalimbali za mkengeuko wa malezi ambazo zimejadiliwa katika sehemu ifuatayo.

### Sababu Zinazohusiana na Wazazi au Walezi

Katika malezi, wazazi au walezi wanao mchango mkubwa katika makuzi na malezi ya watoto na vijana (Burton, Shipps na Gurtis, 2002). Hata hivyo, wazazi na walezi wengi hushindwa kutimiza jukumu la malezi na hivyo kusababisha kilichotarajiwa kuwafikia vijana kushindikana (Cater, Weithorn na Behrman, 1999). Hali hii inapotokea, husababisha mkengeuko wa malezi kutokea. Katika riwaya ya *Rosa Mistika* mkengeuko huu umejitokeza kama inavyoelezwa hapa chini:

### Adhabu za Kupigwa Zinazotolewa na Wazazi

Katika riwaya yaa *Rosa Mistika*, mwaandishi ameonesha jinsi matumizi ya adhabu kubwa kwa watoto kama vile kupigwa na kuchapwa viboko kutoka kwa wazazi yanavyosababisha malezi yanayokusudiwa na wazazi kwa watoto wao kutofikiwa na hivyo kukengeuka. Mwandishi anayaeleza:

> Kabla hajasema lolote alipigwa na kuanguka chini…. “Lete hiyo barua pamoja na shilingi ulizopewa!” Rosa alipigwa tena na tena, makofi yalikwenda mfululizo hata damu ikamtoka puani na mdomoni… Zakaria hakujali; na aliendelea kuunguruma. “Lazima unionyeshe hiyo barua! Rosa akiwa na haya nyingi alichukua mfuko wake wa madaftari, na katika daftari la jiografia alitoa barua hiyo pamoja na shilingi tano. Alimpa baba yake shilingi hizo; lakini ile barua aliikunjakunja na kuitupia mdomoni. Alijaribu kuitafuna lakini baba alimkaba koo. Rosa hakuitema. Zakaria alikaza mkono. Macho ya Rosa yalianza kuwa mekundu, ulimi ulimtoka na barua ilianguka chini. Zakaria aliiokota mara moja. “Sema nani amekupa barua hii!” “Charles” Rosa alitamka kwa shida. (Kezilahabi, 1971:6-7).

Katika dondoo hilo, inaoneshwa namna mzazi anavyotoa adhabu kali ya kupiga kwa mtoto wake kwa makosa ambayo hayastahili adhabu ya kupigwa. Zakaria anampiga na kumdhalilisha binti aliye katika umri wa kubalehe ambapo katika umri huu kwa vijana wengi masuala ya kutongozana ni kawaida (Lenta, 2012). Vijana wanapaswa kufundishwa namna bora ya kuhimili changamoto za

ukuaji. Hata hivyo, Rosa hakuwa na kosa kwani barua iliyokutwa na baba yake kwa Rosa haikuandikwa na Rosa. Hivyo, kama kosa hilo lilistahili adhabu, aliyepaswa kuadhibiwa ni mwandishi wa barua ya mapenzi ambaye ni Charles. Mzazi anajipa mamlaka na uhalali wa kutoa adhabu ya viboko vile atakavyoona inafaa (Scarre, 2003). Hali hii ndiyo inayomsukuma Rosa kuanza kuwaogopa wavulana kama inavyodokezwa "Rosa alikoma kabisa kuwa karibu na wavulana" (uk.9), jambo ambalo si sahihi (Osofsky, 1991). Mwandishi anaionesha hofu ya Rosa kwa wavulana pale anaposema:

> Hivi ndivyo Rosa alivyolelewa; hivi ndivyo alivyotunzwa; hivi ndivyo alivyochungwa na baba yake. Tangu siku hiyo alikoma kutembea na mvulana yeyote. Na Zakaria alipofahamu haya alifurahi sana. Hakufahamu kuwa Rosa alikuwa katika rika baya na kwamba ukali ulikuwa haufai; hakufahamu kwamba mabinti wanahitaji uhuru fulani kutoka kwa baba zao. Hakufahamu kwamba kwa kumpiga binti yake alikuwa akiingilia utawala usio wake…. Hakufahamu kwamba Rosa alihitaji kuwafahamu wavulana. Kwa hiyo, kutokana na malezi ya namna hii, Rosa alianza kuwaangalia wavulana kama watu asiopaswa kuandamana nao au hata kuzungumza nao (Kezilahabi, 1971:9).

Dondoo hilo linoanesha mkengeuko wa malezi wa Rosa unaosababishwa na adhabu na hofu kutoka kwa baba yake. Rosa anawaogopa wavulana na wanaume kama maadui wakubwa wa kumsababishia adhabu ya kupigwa na baba yake. Badala ya kupata maarifa na ujuzi wa namna ya kuishi na kushirikiana na wavulana na wanaume, yeye anajitenga na kuwakimbia. Jambo hili ndilo linamsukuma Rosa kukengeuka malezi kwa kuwa malaya; jambo ambalo linaungwa mkono na Benatar (1998) kuwa adhabu ya kupigwa huwavunja moyo vijana na kuchochea kuendeleza makosa yaleyale. Mwandishi anaeleza hali ya kushindwa kuwamudu wavulana pale anaposema:

> Alipofika kitandani Rosa hakuweza kupata usingizi upesi-alianza kufikiri: 'Kama nikifanya urafiki na wavulana baba yangu atafahamu? Yeye yuko Ukerewe mimi nipo Usukuma. Baba anakaa akinichunga anafikiri yeye atanioa?... Rosa sasa alianza mapenzi. Alianza mapenzi lakini aliyaendea haraka sana kama mbwa aliyekata kamba. Aliona mvulana mmoja au wawili hawamtoshi kwa urafiki. Mwaka huohuo aliwakubalia wavulana watano (Kezilahabi, 1971:32-33).

Nukuu hiyo inaonesha mambo mawili ya mkengeuko wa malezi yanayosababishwa na adhabu ya kupigwa. Kwanza, inaoneshwa mhusika Rosa anaamua kuanza kujihusisha na mapenzi kwa sababu ya kutokuwa na hofu ya kuonwa na baba yake. Jambo la pili linalooneshwa katika nukuu hiyo ni suala la umalaya. Mwandishi anaeleza kuwa Rosa sasa hakuridhishwa na mvulana mmoja au wawili. Alikuwa na wavulana watano. Hitaji la kuwa na wanaume linachochewa na malezi ya ukali wa baba yake na adhabu kali za zuio la kushirikiana na wavulana.

Kwa hivyo, jambo mojawapo linayosukuma mkengeuko wa malezi kwa Rosa linasababishwa na adhabu kali kutoka kwa baba mzazi. Jambo hili linasisitizwa na mwandishi kwa kutumia kisa cha "Kesi ya Rosa Mistika" Mwandishi anapofafanua:

> *(Mungu amekaa juuu ya kiti chake cha enzi. Amevaa miwani mikubwa. Malaika mmoja anapita amebeba karatasi ngumu iliyoandikwa juu "Kesi ya Rosa Mistika").*
>
> MUNGU: Rosa, Kwa nini umejiua?
>
> ROSA: Ee Mungu wangu. Haya yote yametokea kwa sababu ya baba yangu.
>
> *(Baada ya dakika moja, ZAKARIA anaingia. Ana alama nyeusi kifuani. Anamsujudia MUNGU).*
>
> MUNGU: Rosa, ninakuuliza tena, Kwa nini umejiua?
>
> ROSA: Ee Mungu wangu haya yote yametokea kwa sababu ya baba yangu.

| | |
|---|---|
| MUNGU: | Zakaria, una usemi gani kujitetea? |
| ZAKARIA: | Ee Mungu wangu. Haya yote yametokea kwa sababu ya ubaya na udhaifu wake mwenyewe! |
| MUNGU: | Rosa, una ushahidi? |
| ROSA: | Ndiyo, Bwana, Ulimwengu mzima. |
| MUNGU: | (*Anamgeukia ZAKARIA*): Na Zakaria? |
| ZAKARIA: | Ulimwengu mzima, Bwana Mungu wangu |
| | (Kezilahabi, 1971:98). |

Katika dondoo hilo mwandishi anaonesha sababu ya mhusika Rosa kukengeuka malezi kwa kujiua ni baba yake. Makala hii imebaini kuwa adhabu kubwa kwa watoto na vijana pasipo kuelimishwa, huwasukuma vijana hao kukengeuka malezi kwa kuchukua hatua ambazo zinaweza kuleta madhara kwa jamii yao kama alivyokengeka Rosa.

## Ukatili wa Wazazi

Katika maisha ya familia, wazazi wana jukumu la kuwalea watoto wao kwa kufuata taratibu za jamii husika (Korbin, 2003). Hata hivyo, baadhi yao huwakatili watoto na hivyo malezi yaliyokusudiwa kuwafikia hushindikana. Watoto wamekuwa wakifanyiwa ukatili na wazazi kwa namna tofauti (Korbin, 2003). Kwa mfano, katika riwaya ya *Rosa Mistika* mwandishi anaelezea ukatili wa baba kwa watoto wake pale anaposema:

> …Waamshe nataka kuwaona. Zakaria alipoingia ndani ya nyumba wasichana walijifanya kulala; lakini walisikia kila neno alilolisema baba yao. Kwa kuwa Rosa alikuwa amekwisha vunja ungo hakuamshwa. Flora alikuwa darasa la tano aliamshwa Flora, Honorata na Stella waliletwa mbele ya baba yao. Mara moja Zakaria alianza mchezo wake wa kawaida. "Haya ondoeni usingizi! Jipangeni! Nyuma-geu-keni! Nyuma-geu-keni! Nyuma-geu-keni! Jii-ka-zeni! Jii-legezeni! Maark-taim! Shoto kulia shoto kulia. Mikono juu! Chini! Juu! chini… Haya imbeni sasa! *Siku moja wawinda…* aliwaanzishia. Nao hawakuchelewa kuanza (Kezilahabi, 1971:4-5).

Katika dondoo hilo inaoneshwa namna Zakaria anavyowanyanyasa na kuwakatili watoto wake. Zakaria anarudi nyumbani usiku akiwa amelewa na kuwaamsha watoto ili kuwafanyisha gwaride. Watoto wanashurutishwa na wanafanyishwa mazoezi usiku badala ya kulala. Aidha, mtindo huu ulikuwa umezoeleka kwa watoto. Tunafahamishwa hayo kutoka katika kinywa cha mwandishi kwa maneno "Mara moja Zakaria alianza mchezo wake wa kawaida". Jambo hili liliwafanya wamchukie na kumwogopa baba yao badala ya kumheshimu. Watoto baada ya kusikia baba anaingia ndani wanamkimbia na kujifanya wamelala ili wasisumbuliwe na baba yao. Watoto wanamkimbia baba yao kwa kuwa hawamtaki, wanaona ni tishio kwao kimalezi.

Hali hii ni sababu mojawapo ya mkengeuko wa kimalezi wa wazazi kwa watoto kwani watoto hawayapati malezi kwa mzazi anaowakatili ambaye kwa muktadha huu ni baba, au kuyapata malezi yasiyokubalika katika jamii na hivyo kuzua migogoro katika jamii.

## Mtazamo wa Malezi ya Kuchungwa

Katika jamii, wazazi wanapaswa kuwalea watoto wao kiuhalisi na kuwachangamanisha na jamii hizo ili wajue uhalisi wa jamii wanamoishi (Roostin, 2018). Kuwalea watoto tofauti na uhalisi wa maisha katika jamii ni mkengeuko wa kimalezi (Doepke na Zilibotti, 2019). Hali hii inaweza kuwafanya kushindwa kumudu changamoto halisi za jamii wanamoishi na hivyo kuathirika vibaya na changamoto hizo.

Katika riwaya ya *Rosa Mistika* mkengeuko wa kimalezi unaosababishwa na wazazi kuwachunga watoto wao nje ya ulimwengu halisi umejitokeza kupitia wahusika wake. Kwa mfano, mwandishi anaeleza:

> Hivyo ndivyo Rosa alivyolelewa; hivyo ndivyo alivyotunzwa; hivyo ndivyo alivyochungwa. Tangu siku hiyo alikoma kutembea na mvulana yeyote… Kwa hiyo, kutokana na malezi ya namna hiyo, Rosa alianza kuwaangalia wavulana kama watu asiopaswa kuandamana nao, au hata kuzungumza nao (Kezilahabi, 1971:9).

Katika dondoo hilo kunaoneshwa malezi ya kuchungwa anayoyafanya baba yake Rosa kwa binti yake. Rosa anakuzwa katika fikra za kuwaogopa wavulana. Kwa hiyo, kukengeuka kimalezi kwa kufanya umalaya kwa Rosa kunachangiwa na malezi ya baba yake ya kumtenga na wavulana tangu akiwa mdogo. Mwandishi anasimulia jambo hili anaposema:

> Rosa sasa alianza mapenzi. Alianza mapenzi lakini aliyaendea haraka sana kama mbwa aliyekata kamba. Aliona mvulana mmoja au wawili walikuwa hawamtoshi kwa urafiki. Mwaka huohuo aliwakubalia wavulana watano (Kezilahabi, 1971:33).

Maelezo haya yanaonesha Rosa kuingia katika mahusiano ya kimapenzi na wavulana wengi kwa wakati mmoja kwa sababu ya kukosa malezi stahiki kutoka kwa wazazi wake. Baba yake alimchunga na alimtenganisha na wavulana. Lakini Rosa anapogundua kuwa anawahitaji wavulana, anaingia kwa pupa katika mapenzi.

Mwandishi wa riwaya ya *Rosa Mistika* anaendelea kuonesha athari za malezi ya kuchungwa kwa watoto kupitia mhusika Flora na msafiri ndani ya basi pale anaposema:

> Flora ndiye aliyekuwa wa kwanza kuzungumza. "Rosa, shule yetu hii ni ya ajabu. Tunalindwa kama watoto wadogo. Wanafikiri hata wakati wa livu watatuchunga! Wasichana wengi hapa wamekwishapata mimba na kufukuzwa wakati wakiwa hapahapa shuleni"…. Humo basini alisikika kijana mmoja akizungumza kwa sauti. "Shule hii! Hii hapa! Bure sana ingawa wanalindwa. Wanachukuliwa na wapishi wa Wahindi mjini. Kwa sababu ya kulindwalindwa wamekuwa kama wanyama. Wanapenda mtu yeyote yule apataye bahati ya kuonana nao. Wamepoteza uwezo wao wa kuchagua (Kezilahabi, 1971: 62-63).

Katika dondoo hilo mwandishi anapaza sauti kuonesha chagamoto za taasisi za elimu kama vile shule zinavyowalea watoto wa kike kwa kuwafungia na kuwatenga na wavulana. Mwandishi kupitia mhusika Flora anaonekana kupinga hali ya aina hii ya kimalezi. Mwandishi anaonesha kuwa kumnyima uhuru mtoto wa kike kwa kumtenga na jamii ya wavulana kunamsukuma kuutafuta uhuru huo ndani ya shule au wawapo likizo.

### Sababu Zinazohusiana na Watoto au Vijana Wenyewe

Katika malezi, yapo mazingira ambapo wapokeaji wa malezi huamua ama kukiuka au kupuuza kwa makusudi malezi kutoka kwa wazazi au walezi wao (Peterson na Lesch, 2021). Aidha, wakati mwingine wahusika watoto na vijana huamua kufuata wanachokitaka wao hata kama kwa kufanya hivyo wanakengeuka (Yeager, 2017). Kwa jumla, matukio yote yanayohusu ukengeukaji wa malezi katika hali hii ndiyo katika makala hii yanatazamwa kama sababu zinazotokana na watoto au vijana wenyewe. Sababu za mikengeuko hiyo ya kimalezi imejadiliwa hapa chini:

#### Msukumo wa Kutaka Mabadiliko

Katika jamii, yapo mazingira ambamo vijana hutaka mabadiliko ili kuendana na wakati wao (Wang na Khalis, 2014). Vijana hujikuta wanataka mabadiliko ambayo wanafikiri yatawaweka huru (Yeager, 2017). Katika harakati za kuyataka mabadiliko haya ndipo wanajikuta wakikengeuka malezi.

Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, mwandishi anamtumia mhusika Mkuu wa Wilaya kwenda nyumbani kwa Zakaria kumchukua Rosa ili waende kufanya starehe ufukweni; na Rosa anaamua kuondoka nyumbani licha ya kukataliwa na baba yake. Hali hii inasababisha mkengeuko wa malezi kwa vijana hawa dhidi ya wazazi na jamii zao. Mwandishi anaeleza:

> ….Zakaria alipotoka nje alimfokea sana Mkuu wa Wilaya. "Rudi na motokaa yako! Na wewe Rosa usitoe pua yako nje! Nisikuone unatoka hapa! …. Rosa alitoka nje ghafla. Alitapika maneno. "Kila wakati unatuchunga. Unafikiri utatuoa wewe!" Zakaria aliyapata yote …. Mkuu wa Wilaya alikuwa pale kushuhudia. Zakaria kutunza heshima yake, alifunua mdomo. Maneno fulani yalitoka mdomoni mwake. "Rosa, tangu leo wewe si mtoto wangu" "Tangu leo wewe si baba yangu" Rosa alidakia bila kukawia. Aliingia mara moja ndani ya motokaa na kwenda zake *Beach*. Siku hiyo Rosa hakurudi nyumbani (Kezilahabi, 1971:58).

Katika dondoo hilo inaoneshwa namna Rosa anavyotaka mabadiliko na kusababisha kutukanana na baba yake. Rosa hataki malezi ya kulindwa na kuchungwa na baba yake ambayo ndiyo malezi yaliyomkuza. Rosa anamwonesha baba yake kuwa hataki malezi ya awali ambayo ndiyo yaliyozoeleka katika famila ya Zakaria.

Kitendo kingine cha Rosa kinachoonesha hali ya kutaka mabadiliko ni kitendo cha kutoka na mwanamume kwenda kutembea ili kufanya starehe ufukweni pamoja na kulala nje ya nyumbani. Jambo la kutembea na wanaume na kulala nje ya nyumbani lilikuwa mwiko mkubwa katika familia ya Zakaria. Rosa anafanya makusudi ili kukataa malezi aliyokuzwa nayo kwa kuwa malezi hayo anaona hayampi uhuru.

**Kunyimwa Uhuru**

Binadamu anahitaji uhuru binafsi wa kuamua kufanya mambo yake hasa kulingana na fikra zake au pale anapogundua kuwa kile anachokifanya si kosa katika jamii yake (Achtenberg, 2014). Vijana wamekuwa wakinyimwa uhuru na aidha, wazazi au walezi wao au taasisi walimo vijana hao na hivyo kuamua kuutafuta uhuru kwa nguvu zao ili kufikia malengo yao (Anker, 2014). Katika harakati za kuutafuta uhuru, vijana wamekuwa wakijikuta katika mtego wa kuyakengeuka malezi (Schut na Grassiani, 2017)

Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, Rosa ananyimwa uhuru wa kuchangamana na kushirikiana na wavulana tangu akiwa mdogo. Jambo hili linamsukuma kukengeuka kimalezi na kuwa malaya baada ya kujua kuwa anawahitaji wanaume. Mwandishi anasema:

> Hivyo ndivyo Rosa alivyolelewa; hivyo ndivyo alivyotunzwa; hivyo ndivyo alivyochungwa na baba yake. Tangu siku hiyo alikoma kutembea na mvulana yoyote…. Zakaria hakufahamu kwamba Rosa alikuwa katika rika baya, na kwamba ukali ulikuwa haufai; hakufahamu kwamba mabinti wanahitaji uhuru fulani kutoka kwa baba zao; hakufahamu kwamba kwa kumpiga bintiye alikuwa akiingilia utawala usio wake na kwamba kuhusu maoni ya ndoa yeye alifaa kidogo sana na hakufahamu kwamba Rosa alihitaji kuwafahamu wavulana. Kwa hiyo, kutokana na malezi ya aina hii Rosa alianza kuwaona wavulana kama watu asiopaswa kuandamana nao, na hata kuzungumza nao (Kezilahabi, 1971:9).

Dondoo hilo linaonesha namna Rosa anavyonyimwa uhuru wa kushirikiana na wavulana katika majukumu ya kawaida katika jamii yao. Jambo hili linamsukuma kukengeuka kwa kuwa malaya katika maisha yake ya baadaye anapojikuta kuwa ulimwengu halisi unampasa kushirikiana na wanaume. Rosa anashindwa kumudu changamoto za mahusiano ya kimapenzi na kuwa malaya kwa sababu ya kuutafuta uhuru alioukosa kwa kunyimwa na wazazi wake. Mwandishi anaeleza:

> …. Barua yenyewe ilikuwa ya mapenzi na ilikuwa ikimwomba kidole cha pete. Rosa aliona kwamba hawezi kupoteza bahati yake. Alifikiri kwamba mwanaume wa kwanza kuonesha mapenzi ndiye yeye atakayemwoa. Rosa alikubali. Alijibu barua hiyo kwa upole sana. Rosa sasa alianza mapenzi. Alianza mapenzi lakini aliyaendea haraka sana kama mbwa aliyekata kamba. Aliona mvulana mmoja au

> wawili hawamtoshi kwa urafiki. Mwaka huo huo aliwakubali wavulana watano (Kezilahabi 1971:33).

Nukuu hiyo inatuonesha namna Rosa anavyowataka wanaume kwa nguvu na juhudi zote. Rosa anawataka wanaume kwa kasi kwa sababu alinyimwa uhuru wa kuwa nao. Rosa anavyotambua kuwa anawahitaji wanaume, anakwenda kwa kasi na kukubali wanaume pasipo kuwa na stadi za kuwafahamu wavulana; jambo linalomfanya Rosa kuwa malaya.

### Msukumo wa Makundi-rika

Vijana huweza kuwa wanashirikiana na wenzao wa makundi tofautitofauti wenye rika linalolingana (Burke na Sass, 2013). Makundi haya huwa na tabia tofauti za kimalezi kutoka katika familia na jamii zao. Tofauti za kimalezi miongoni mwa vijana katika makundi huweza kuathiriana miongoni mwa vijana husika (Li na Guo, 2016). Athari hizo huweza kuwa mbaya zinazochochea mkengeuko wa malezi kwa wengine.

Katika riwaya ya *Rosa Mistika* kwa mfano, Rosa anaanza kukengeuka malezi ya baba na familia yake kwa kuanza kufikiria kujihusisha na wanaume kwa sababu ya nguvu ya makundi-rika. Mwandishi anaeleza:

> …. Alipoingia darasa la kumi na moja Rosa alikuwa bado akijifikiria yeye kwamba aliweza kujitosheleza…. Rosa alikuwa amesimama kwenye kituo cha basi akingojea basi la kwenda Rosary College lifike, na karibu naye kulikuwa na wavulana wawili wakizungumza kwa sauti ya juu. Rosa aliudhika aliposikia jina lake likitajwa. Wale vijana walikuwa hawajamwona. Rosa alisikiliza kwa makini. "Nasikia msichana huyo hapendi kuzungumza na wavulana!" "Sijui anajifikiria yeye nani?" "Nafikiri anamwogopa baba yake" "Nasikia baba yake mkali sana?" "Sana! Alitutandika viboko bwana." "John alikuwa anasema kwamba msichana huyo ni kilema." Hakuna uzuri usio na dosari." "Kweli bwana inawezekana. Wewe unafikiri msichana anaweza kufika darasa la kumi na moja bila…" Rosa hakusikia vizuri maneno yaliyosemwa mwishoni. Aliona wale vijana wakipanda basi kuelekea Bwiru. Maneno hayo yalimkata ini. Yalimsumbua sana moyoni. Alianza kufikiri…. Wanasema kwamba mimi kilema! Nimekosa nini? Walikuwa wanamaanisha nini waliposema kwamba mimi ni kilema?.... hata alipokuwa kitandani maneno yale yaliendelea kuzunguka kichwani mwake. Alikata shauri. Alikata shauri kwenda kucheza dansi (Kezilahabi, 1971:29-30).

Katika dondoo hilo inaoneshwa nguvu ya mazungumzo ya vijana yanavyomwathiri Rosa ambaye hadi sasa akiwa darasa la kumi na moja alikuwa anaendelea kuwa mtii wa malezi ya familia na ya shule yake. Rosa anaanza kusukumwa kuwa kinyume na malezi ya familia na shule kutokana na msukumo wa mazungumzo ya vijana wenzake. Rosa anajisikia vibaya kusikia kwamba yeye ni kilema kwa kutokuwa na wavulana. Msukumo huo unamsumbua Rosa na kuanza kujiona labda ana kasoro na hivyo kujiingiza katika kukengeuka.

### Sababu za Kijamii

Katika jamii, watu hujikuta wakihusika katika taasisi mbalimbali za kijamii kama vile shule, vyuo na taasisi za dini. Jamii na taasisi zake ambazo vijana hupitia, huweza kumsukuma mhusika kukengeuka malezi. Wahusika wameoneshwa wakipitia katika mazingira tofauti ya kijamii yenye mchango wake wa malezi. Mchango huo wa malezi unapopuuzwa au kutotolewa huathiri maendeleo kwa mhusika. Kwa hiyo, katika muktadha huu, mhusika hukengeuka malezi kutokana na ama changamoto mbalimbali katika mazingira ya jamii yake au kushindwa kwa taasisi anazopitia mhusika katika jamii yake. Sababu hizo zimejadiliwa kama ifuatavyo:

## Athari za Umagharibi

Mkengeuko mwingine wa kimalezi unaosababishwa na jamii ni ule unaotokana na athari za Umagharibi kwa wahusika (Faleiro, 2012). Nyenzo kubwa inayoathiri wahusika ni elimu ya Kimagharibi (Daniel na Nagar, 2016). Mathalani, katika riwaya ya *Rosa Mistika* wahusika vijana wengi waliopata elimu ya Kimagharibi wameonekana kugombana na wazazi wao kutokana na kupinga au kuacha malezi waliyopata kwa wazazi wao. Mwandishi anaeleza:

> Ndalo, ulimwengu umebadilika."
>
> "Kwa nini?"
>
> "Leo hii binti yangu kaniasi. Amesema kwamba tangu leo mimi si baba yake!"
>
> Tena kaniambia mbele ya Mkuu wa Wilaya. Macho kwa macho."
>
> "Sema kweli!"
>
> "Aaah! Wewe unafikiri uongo!"
>
> "Kwa kweli hata mimi mwenyewe ninashangaa. Wewe si mtu wa kwanza kutendewa jambo kama hili. Juzijuzi mzee fulani kaambiwa hivihivi na binti yake, eti kwa sababu alimzuia kuvaa nguo zao hizi za siku hizi …'teti'… 'tahiti'… 'taiti ee ndiyo, 'taiti'.
>
> Mzee mwingine nimemsikia huko Bulamba. Yeye alijichoma ulimi kwa sababu ya kulazimishwa na mtoto wake kutumia uma. Labda ingalifaa kama tusingaliwapeleka watoto wetu shuleni." (Kezilahabi, 1971:58-59).

Katika dondoo hilo inaoneshwa namna vijana waliosoma wanavyogombana na familia zao kwa kukengeuka malezi asilia baada ya kwenda shule na kupata elimu ya Kimagharibi. Katika dondoo hilo mhusika Zakaria analalamika kwa Mzee Ndalo namna alivyotukanwa na kukanwa na binti yake Rosa kuwa yeye si baba yake. Aidha, taarifa za vijana waliosoma kuwakana baba zao kunaoneshwa kuwa ni jambo la kawaida kwani hata mhusika Mzee Ndalo anathibitisha kuwa amesikia kwa ndugu zake wengine kukataliwa. Watoto wanawakana wazazi hadharani kwa mambo ambayo ni ya kawaida. Mathalani, kuzuiwa kuvaa nguo zisizositiri mwili na kuzuiwa kwenda kufanya starehe.

Makala hii imebaini kuwa elimu ya Kimagharibi na mitindo ya maisha ya Kimagharibi imeathiri malezi ya vijana wengi kupitia shule na vyuo. Vijana wengi waliosoma hushindwa kuzitumia elimu hizo kwa mtindo chanya ili kuzikomboa jamii na familia zao. Kwa mfano, Rosa anamkana baba yake baada ya kupata elimu ya Kimagharibi. Rosa anabadilika baada ya kutoka mikononi mwa familia yake na kupitia mabadiliko hayo ndiyo yanamsukuma kumkana baba yake baada ya kumzuia kwenda kutembea na kufanya starehe na Mkuu wa Wilaya.

Kwa upande mwingine, makala hii inaona nafasi duni ya wakuu wanaoteuliwa kusimamia serikali. Kwa mfano, inaelezwa kuwa, Rosa anamkana baba yake mbele ya Mkuu wa Wilaya lakini hatuoni hatua zozote zinazochukuliwa na Mkuu huyo wa Wilaya kukemea au kuchukua hatua. Mkuu wa Wilaya anaungana na Rosa kudharau malezi ya wazazi.

Kwa hiyo, misukumo ya jamii kupitia elimu ya Kimagharibi huweza kuwakengeusha wahusika kimalezi kama inavyoonekana katika maelezo ya hapo juu. Suala hili limeoneshwa na waandishi kwa kuwa lipo katika jamii.

## Taasisi Zinazohusika na Malezi Kushindwa Kutimiza Wajibu

Katika jamii, zipo taasisi mbalimbali ambazo watoto na vijama hupitia. Tasisi hizi ni pamoja na shule, vyuo, dini, taasisi za ustawi na maendeleo ya jamii na nyinginezo nyingi (Martin, 1968). Taasisi hizi zinawajibika kuendeleza malezi kwa watoto na vijana ili wakue katika muelekeo chanya wa malezi kwa manufaa ya jamii (Herbbar na Acharya, 2003). Licha ya kuwapo kwake na umuhimu wake, taasisi hizi zimekuwa zikishindwa kutekeleza majukumu ya kimalezi kwa watoto na vijana na hivyo kuwafanya kukengeuka malezi.

Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, kunaoneshwa baadhi ya taasisi za malezi zinavyoshindwa kutimiza majukumu yao kama anavyoeleza mwandishi katika taasisi ya shule ya Rosary alikokuwa akisoama Rosa. Mwandishi anaeleza haya anaposema:

> Unafahamu Thereza siku hizi ninawachezea wavulana kama mtu aendeshaye punda…. Huyu hapa mwenye kofia kichwani jina lake Deogratias…. Thereza aliangalia kwa mshangao. Rafiki yake aliyekuwa akimuona mjinga zamani, katia fora. “Mbona kama mimi ningekuwa nataka ningekuwa na arobaini sasa, lakini wengine nimewakataa nimebakiza wawili tu…. Wakati huu wasichana walikuwa wameshamshangilia sana Rosa. Aligeuka kupindukia. Katika mtihani wa kuingia darasa la kumi na mbili alikuwa wa ishirini. Alianza kupoteza muda wake mwingi si tu kwa kufuma na kushona vitambaa, lakini sasa mara nyingine alikuwa analala mjini. Masista walishangaa kumwona Rosa anatelemka sana katika mitihani yake…. Siku moja alipoletwa kutoka mjini kwa gari la mtu aliyeonekana kuwa mwenye cheo, Rosa alishangaa kumkuta Sista John akimngojea. Alikuwa amepigiwa simu. “Utaniona kesho asubuhi ofisini,” Sista John alisema kwa ukali…. Asubuhi Rosa alipoingia ofisini alikuwa anatetemeka kwa hofu. Sista John siku hiyo hakucheka wala hakuwa na haja ya kumzungumzisha maneno mengi.
>
> “Rosa,” Sista aliita
>
> “Sista”
>
> “Nani aliyekuleta kwa gari?”
>
> “Rafiki yangu, anafanya kazi benki.”
>
> “Una rafiki mwingine?”
>
> “Ndiyo”
>
> “Nani?”
>
> “Deogratias.”
>
> “Deogratias! Deogratias! Rosa, tumekusudia kukupeleka nyumbani. Utarudi tu kufanya mtihani wako wa *Cambridge*”. Rosa alilia lakini Sista John akisema amesema. Alikuwa akifanya kazi yake. Rosa alikwenda nyumbani (Kezilahabi, 1971:33-36).

Katika dondo hilo kunadokezwa kubadilika kwa wanafuzi wengi kimalezi wanapofika shuleni. Wanafunzi wengi wanabadilika kwa kukengeuka kwa kuwa malaya baada ya kufika shuleni kama vile Rosa na Thereza. Kwa mfano, Rosa ambaye hakuwa na mahusiano ya kimapenzi na mtu mwingine, sasa anaonekana kubadilika kwa kukengeuka malezi aliyokuja nayo kutoka nyumbani kwao na kuwa malaya kwa kujihusisha na wanaume wengi wa umri mkubwa kama vile mfanyakazi wa benki pamoja na Deogratiasi. Kitendo cha wasichana wa shule ya Rosary kuwa malaya tofauti na walivyokuja awali kutoka katika familia zao kama ilivyokuwa kwa Rosa, kunaonesha kushindwa kwa uongozi wa taasisi ya shule hiyo ambayo huhusika katika malezi. Badala ya shule kuendeleza malezi bora kutoka kwa wazazi wa watoto wao, shule inashindwa na hivyo kuwafanya kubadilika kwa kukengeuka kimalezi.

Kosa jingine la kimalezi linalofanywa na shule kupitia kwa Sista John ni kumfukuza shule Rosa. Shule inashughulika na matokeo ya mtu mmojammoja pasipo kuchunguza chanzo cha matokeo hayo. Kimsingi, wanafunzi wengi kutoka katika shule aliyokuwa akisoma Rosa walikuwa wakijihusisha na masuala ya kimapenzi kwa kutoroka shule kwa siri kama ilivyokuwa kwa Rosa na Thereza. Hata hivyo, Rosa alichelewa kujiunga nao na anapoingia, anakuwa kwa kasi na kuwapiku rafiki zake akiwamo Thereza. Hivyo, kitendo cha Rosa kufukuzwa hakikuwa suluhisho kwa wengine waliobaki. kulitarajiwa shule kutafuta sababu na mbinu wanazotumia wanafunzi kutoroka na namna ya kuzizuia, tofauti na walivyomfukuza Rosa. Kwa kufanya hivi, uongozi wa taasisi hii ya kijamii umeshindwa

kutekeleza majukumu yake ya kimalezi na hivi kufanya wanafuzi wake kukengeuka malezi. Uongozi wa taasisi hii ya shule unachukua jukumu la kumfukuza Rosa hata pale Rosa anapotaja waliohusika kumfanya kukengeuka malezi kwa kufanya umalaya na kulala nje ya shule ambao ni mfanyakazi wa benki na Deogratias ambaye ni mkuu ya taasisi ya Maendeleo ya Jamii. Hakuonekani hatua zozote za taasisi zinazochukuliwa kwa wahusika waliomsababisha Rosa kukengeuka badala yake wanamfukuza Rosa na kuwaacha waharibifu wa wanafunzi wao wakiendelea na mchezo wao wa kuharibu wengine.

Tofauti na shule na wafanyakazi wa benki, taasisi nyingine zinazohusika katika kukengeusha malezi kwa vijana katika riwaya ya *Rosa Mistika* ni taasisi ya Maendeleo ya Jamii iliyokuwa ikiongozwa na Deogratias. Mhusika Deogratias aliyekuwa mkuu wa taasisi hii alikuwa ni miongoni mwa watu waliokuwa wakihusika katika kuwakengeusha watoto wa shule kwa kufanya nao umalaya. Mwandishi anaeleza haya pale anaposema:

> Akiwa na miaka arobaini na miwili alikuwa bado akiwaandikia barua wasichana akisema, "Ninakupenda kama almasi ya Mwadui."…. Huyu ndiye alikuwa Deogratias: Bwana Maendeleo. Zaidi ya hayo, Deogratias alikuwa mmoja kati ya wale watu watumiao vyeo vyao na pesa zao kupata chochote wapendacho. Utawasikia mara nyingi wakipiga kelele juu ya jukwaa, utafikiri mwisho wa dunia ….Wakishuka kutoka jukwaani utaona baadaye benzi zao zikipeleka watoto "*beach*". Wazee wa mabinti hawa hawana la kusema. Watasema nini hali mkubwa amekwisha penda? Kijana gani atawazungumzia wasichana hao? Nzi hatui juu ya damu ya simba. Habari zilivuma kuwa Deogratias aliwahamisha wazee wawili kutoka Mwanza kwa sababu ya kupinga asiwachukue binti zao. Vijana wengi walitafutiwa sababu za kuwekwa jela. Deogratias alipenda sana dansi, hasa zile za watoto wa shule. Alizoea kwenda na kofia …. Hivi ndivyo alivyowatafuta wale wenye joto bado. Kwa wakati huu alikuwa akihitaji mwanamke wa tatu na bahati alikuwa amekwisha ipata. Ilikuwa siku ya kwanza Rosa kushikwa mikononi mwa mwanamume yoyote. 'Malezi mema' yalimfanya apende yule mwanamume wa kwanza kuonana naye (Kezilahabi, 1971:41).

Dondoo hilo linaonesha namna uongozi wa taasisi zinazohusika na malezi zinavyotumika kukengeuka na kukengeusha malezi ya watoto na vijana. Deogratias, Bwana Maendeleo anajihusisha na kuwarubuni wasichana wa shule ili afanye nao mapenzi badala ya yeye kuwa mstari wa mbele kukemea jambo hili. Deogratias anapingana na mahubiri anayoyatoa jukwaani kuhusu vijana wanaojihusisha na mapenzi na watoto wa shule na badala yake yeye ndiye anayehusika kuwarubuni wasichana wa shule. Aidha, Deogratias anawatishia wazazi wa wasichana na vijana kwa kuwahamisha mji au kuwaweka jela.

Hila nyingine anayoifanya Deogratias kwa kutumia ofisi yake ni kutumia madaraka yake ya malezi vibaya. Deogratias anatumia mamlaka yake kuwahamisha mji wazee wanaopingana naye katika masuala ya kuwakengeusha vijana wao kwa kushirikiana nao kimapenzi. Pia, Deogratias anawaweka jela vijana pasipo sababau ili kutimiza malengo ya kuwatumia wasichana atakavyo. Jambo hili linawafanya wazazi na jamii anayoiongoza Deogratias kumwogopa na hivyo yeye kuendelea kufanya atakalo kwa kutumia pesa, mali na magari ya ofisi yake kutimiza atakalo. Hali hii ndiyo inayomfanya ampate Rosa, msichana aliyekuwa amelelewa pasipo kukutana na mwanamume yeyote tangu utotoni mwake. Badala ya Deogratias kumsaidia Rosa na wanafunzi wengine kutunza na kuendeleza malezi mema, yeye anakuwa mstari wa mbele kuwafanya wasichana hawa kukengeuka kwa kuwaingiza katika mapenzi huku wakiwa bado wanafunzi.

Makala hii imebaini kuwa taasisi na viongozi wa taasisi mbalimbali zinazohusika na malezi huweza kutumika kukengeusha watu malezi kama ilivyo katika taasisi ya shule, benki na taasisi ya Maendeleo tuliyojadili hapo juu. Aidha, viongozi wa taasisi mbalimbali huweza kutumia fedha, mali, magari ya kifahari pamoja na mamlaka yao walionayo kufanya jambo lolote watakalo hata kama ni la kukengeuka malezi bila ya kuingiliwa na nguvu nyinginezo.

**Hitimisho**

Katika makala hii kumejadiliwa sababu za wahusika katika riwaya ya *Rosa Mistika* kukengeuka malezi. Imeonekana kuwa, mkengeuko wa malezi unaweza kusababishwa na pande kuu tatu. Upande wa kwaza ni wa wazazi au walezi wa watoto na vijana kwa kutotimiza wajibu wao wa kimalezi; yaani kile kinachokusudiwa kutoka kwa wazazi au walezi kutofika kwa sababu za makosa ya wazazi. Pili, vijana na watoto kushindwa kufuata taratibu za kimalezi walizozipata kutoka kwa wazazi wao. Tatu, jamii kushindwa kuendeleza malezi kutoka kwa wazazi na watoto katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya kijamii. Sababu zote hizi za kimalezi zimefumbatwa katika mambo makuu mbalimbali ambayo ni pamoja na wakati, umri, jinsi, mazingira, muktadha, jamii mahususi na utandawazi.

**Marejeleo**


Achtenberg, D. (2014). "Plato and Levinas on Relations to the other Assential Vulnerabilities" katika *Freedom*: 40-70.

Anker, E. (2014) ."Freedom and the Human in Evolutionary Political Theory". *Political Research Quarterly*, Juz. 2: 453-456.

BAKITA, (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Longhorn Publishers Ltd.

BAKIZA, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.

Beebee, T.O. (2016). *The Ethics of World Literature*. The Pennsylvania State University.

Benatar, D. (1998). "Corporal Punishment". Sociological Theory and Practise. Florida State University Depertment of Philosophy. Juz. 24, No. 2, kur. 237-260.

Burke, M.A. na Sass, T.R. (2013). "Classroom Peer Effects and Student Achievement". *Journal of Labour Economics*, Juz.31(1): 51-82.

Burton, P. Shipps, S. na Curtis, L. (2002). "All in the Family: A Simultaneous Model of Parenting Style and Child Conduct". *The American Economic Review*, Juz. 92 (2): 368-372.

Carter, M. J. na Carter, S. (2014). "How Thim in Literature can Inform Sociological Theory, Research and Teaching". *Springer Science + Business Media*.Juz. 45 (4): 388-411.

Cater, L. S, Weithorn L.A. na Behrman E.R. (1999). "Domestic Violence and Children: Analysis and Recommendations". *The Future of Children*, Juz. 19 (3): 4-20.

Coser, L. (1963). *Sociology through Literature: An Introductory Reader*. Englewood Cliffs: Prentice Hall.

Daniel, R. na Nagar, D. (2016). *Africa and External Actors*. Cape Town, South Africa: Centre for Conflict Resolution.

Doepke, M. na Zilibotti, F. (2019). "The Economic roots of Helicopter Parenting". *The Phi Delter Kappan*: Juz.100 (7): 22-27.

Duric, M. na Bunijevac, M. (2017). "Parental Involvement as a Important Factor for Successful Education". *C.E.P.S Jonal*. Juz. 7 (3): 137-153.

Faleiro, E. (2012). "Colonialism, Neo-Colonialism and Beyound". *World Affairs: The Journal of International Issues*, Juz.16 (4): 12-23

Hallen, G. C. (1966). "Sociology of Literature". *Pi Gamma Mu, International Honor*, Juz. 41(1): 12-18.

Hamilton, L. (Mh) (2012). "Freedom and Power I". *Theoria: A Journal of Social and Political Theory*, Juz.59 (131): V-Viii.

Hebbar, R na Acharya, S. (2003). "Social Institution and Development Challenges". *Economic and Political Weekly*, Juz. 38 (32): 3343-3346.

Jonas, M. (2017). "Resentment of Advice and Norms of Advice" *Ethical Theory and Moral Practice*, Juz. 20 (4): 813-828.

Kezilahabi, E (1971) *Rosa Mistika*. Dar es Salaam: East Africa Literature Bureau..

Korbin, J.E. (2003). "Children, Childhood and Violence". *Annual Review of Anthropology*, Juz.32: 431-446.

Lenta, P. (2012). "Corporal Punishment of Children". *Sociological Theory and Practise*, Juz. 38 (4): 689-716

Li, Y na Guo, G. (2016). "Peer Influence on Aggressive Behaviour, Smoking and Sexual Behaviour: A Study of Rondomly-assigned Colledge Roommates". *Journal of Health and Social Behaviour*, Juz. 57 (3): 297-318.

Madumulla, J.S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Limited.

Mahonge, F. R. (2016). *The Representation of Masculinity in Euphrase Kezilahabi's Novels*. PhD Thesis in Literature (Haijachapishwa), Moi University, Kenya.

Martin, C. (2017). "Parenting as a public Problem in a Neoliberal Era: A changing Regime in France?" *Journal of Comparative Family Studies*, Juz. 48 (3): 303-314.

Martin, T. W. (1968). "Social Institutions: A Refomulation of the Concept". *The Pacific Sociological Review*, Juz.11 (2):100-109.

Mbatiah, M. (2012). "Riwaya ya Kiswahili kama Tahakiki ya Jamii Baada-Ukoloni", *Kioo Cha Lugha*, Juz. 10: 95-101.

Mbatiah, M. (2016). *Riwaya ya Kiswahili*: Chimbuko na Maendeleo yake. Nairobi Kenya:The Jomo Kenyata Foundation.

Mlacha, S. A. K. (1986). "The Identification of Personality Differences in Kiswahili Prose fiction", *Kiswahili*: 146-169.

Mlacha, S. A. K. (1989). "The Use of Metaphors in Kezilahabi's Novel: Rosa Mistika", *Kiswahili*: 25-31.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTU.

Ondieki, F. M. (2015). *Usawiri wa Watoto Katika Riwaya za Kiswahili Zilizoandikwa na Mohamed Suleiman Mohamed na Euphrase Kezilahabi*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.

Osofsky, D. J. (1999). "The Impact of Violence on Children". *The Future of Children*, Juz. 9 (3): 33-49.

Petersen, J. M na Lesch, E. (2021). "A Child Needs Both Mother and aFather". *Journal of Comperative family studies*, Juz. 52 (4): 715-742.

Roostin, E. (2018). "Family Influence on the Development of Children". *Jounal of Elementary Education*. Juz. 2 (1): 1-12.

Sanga, D. (2018). "Moral Panic: Hidden Stories of Kangamoko Dancers in Dar es Salaa Tanzania". *Kioo cha Lugha*, Juz. 16: 81-94.

Scarre, G. (2003). "Corporal Punishment". *Ethical Theory and Moral Practice*, Juz.6 (3): 295-316.

Schut, T and Grassiani, E. (2017). "Introduction: Freedom". *Etnofoor*, Juz. 29 (1): 7-10.

Titus, S. (2018). *Georg Lukacs. The Standard Encyclopedia of Philosophy*. Metaphysics Research Lab. USA: Stanford University.

TUKI, (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi Kenya: Oxford University Press.

Wamitila, K. W. (2008) *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi Kenya: Vide-Muwa Publishers Limited.

Wang, M. na Khalil, S. (2014). "Does Parental Involvement Matter for Student Achievment and Mental Heath in High School?" *Child Development*, Juz. 85 (2): 610-625.

Wanjala, J.A. (2015). *Usawiri wa Malezi Unavyoathiri Utambulisho wa Vijana katika Riwaya ya Kiswahili*. Tasnifu ya M.A Sanaa (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi Kenya.

Yeager, D. S. (2017). "Social and Emotional Learning Programs for Adolescents". *The Future of Children*, Juz. 27 (1): 73-94.